CHUO KIKUU CHA SOKOINE CHA KILIMO

# MATUKIO YA SUA

*Oktoba - Desemba, 2025*



Toleo la 20

Ardhi ni Hazina

# Yaliyomo


| | |
|---|---|
| 1 | Bodi ya Uhariri. |
| 2 | Mwenyekiti wa Baraza la SUA atoa wito wa kutumia tafiti kuchochea maendeleo |
| 3 | Prof. Chibunda awataka wahitimu wa SUA kuwa wajasiri na wabunifu |
| 4 | Elimu ya Kilimo Ni Nguzo Kuu Kukabiliana na Changamoto za Chakula na Ajira |
| 5 | SUA yaanzisha mageuzi makubwa ya mitaala kuimarisha ujuzi wa vitendo |
| 6 | Wananchi wa Mpimbwe waiomba SUA kuwashauri namna sahihi ya kulima mpunga pamoja na kujua mbegu nzuri. |
| 7 | Uandishi wa machapisho ya kisayansi wapewa kipaumbele SUA |
| 8 | SUA yalipa fidia ya Bilioni 1.7 Mpimbwe mkoani Katavi |
| 9 | Wanafunzi watatu SUA wang'ara tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari za Sayansi Tanzania |
| 10 | Tafiti zitachochea kilimo Ikolojia kwa maendeleo endelevu, Prof. Mwatawala |
| 11 | • Elimu, Msingi wa Kudhibiti Mabadiliko ya Tabianchi<br>• Wataalam wa Lugha Kutoka Cuba Waanza Kufundisha Kihispania SUA, Waongeza Nguvu katika Ushirikiano wa Kimataifa |
| 12 | Ugonjwa wa homa ya kiwele wapunguza mapato ya wafugaji wa ng'ombe wa maziwa |
| 13 | SUA yajipanga kutoa wahitimu wenye ujuzi na wenye kuendana na mahitaji ya soko |
| 14 | • Vijana washauriwa kutumia maarifa yanayotolewa SUA kujiinua kimaisha<br>• Warsha ya Uzinduzi wa Mradi wa Mtandao wa Wadau wa Utafiti wa Kilimo Ikolojia kwa Afrika Mashariki (Regional Multi-Actor Research Network on Agroecology in East Africa - RMRN-EA) inalenga Kuimarisha Kilimo ikolojia Afrika Mashariki. |
| 15 | Ubunifu na Utafiti Nguzo za Maendeleo ya Jamii |
| 16 | SUA yawapa elimu na pongezi wanafunzi wa mwaka kwanza 2025/2026 |
| 17 | TRA yaitembelea SUA kujifunza kuhusu uwekezaji katika kilimo |
| 18 | SUA imeenda na kasi ya mabadiliko ya Sera ya Elimu - TCU |
| 19 | Ufugaji wa kuku una mchango katika kuondoa umaskini |
| 20 | SUA yashirikiana na Ashish Life Science kuwatambua wanafunzi bora wa tiba ya wanyama |
| 21 | SUA na Mzuri Africa washirikiana kukuza ujuzi wa vitendo kwa wanafunzi |
| 22 | Ubunifu na uthubutu msingi katika maendeleo yenu, Prof. Mwatawala |
| 24 | Nishati jadidifu kuboresha shughuli za kilimo nchini |

# BODI YA UHARIRI


## WATAALAMU WA MAWASILIANO NA MASOKO

Bi. Suzana Magobeko
**Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Masoko**


Bw. Asifiwe Mbembela
**Afisa Mawasiliano na Masoko**

## MHARIRI

Prof. James Nyangas
**Mkuu wa Idara ya Elimu ya Saikolojia na Unasihi.**

## WASANIFU

Bw. Rajab Kimaro
Bi. Jackline Japhet



# Mwenyekiti wa Baraza la SUA atoa wito wa kutumia tafiti kuchochea maendeleo

Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Bw. Andrew Wilson, amehimiza matumizi ya matokeo ya tafiti katika kutunga sera na mipango ya maendeleo ya taifa, akisema tafiti hizo zina mchango mkubwa katika kukuza uchumi na ustawi wa jamii.

Alisema SUA inaendesha miradi 36 ya kitafiti yenye thamani ya shilingi bilioni 10.5, ikihusisha ufadhili kutoka kwa wadau wa kimataifa, COSTECH na mapato ya ndani ya chuo.

Bw. Wilson alibainisha kuwa Baraza linafuatilia kwa karibu utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Chuo 2021–2026, ambao hadi sasa umefikia asilimia 85, sambamba na kuhakikisha matumizi sahihi ya rasilimali, uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa fedha.

Alisisitiza kuwa kupitia shughuli za utafiti na usimamizi bora wa rasilimali, SUA itaendelea kuwa taasisi mahiri ya elimu, utafiti na huduma kwa jamii.





# Prof. Chibunda awataka wahitimu wa SUA kuwa wajasiri na wabunifu

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Prof. Raphael Chibunda, amewataka wahitimu wa chuo hicho kutumia maarifa waliyojipatia kwa ujasiri, ubunifu na uwajibikaji katika kutatua changamoto za jamii na kuchangia maendeleo ya taifa.

Akizungumza wakati wa mahafali ya 46 ya SUA yaliyofanyika katika Kampasi ya Edward Moringe, Morogoro, Prof. Chibunda alisema elimu wanayoipata wanafunzi inapaswa kuwa chachu ya mageuzi chanya katika jamii kupitia matumizi ya ujuzi na teknolojia bunifu.

"Tunawaamini ninyi kama kizazi cha mabadiliko. Nendeni mkayatumie maarifa mliyopata siyo tu kutafuta ajira, bali kubuni ajira na kutatua changamoto zinazolikabili taifa letu," alisema Prof. Chibunda.

Alisema katika mahafali hayo, kulikuwa na jumla ya programu 85 ambazo zilitoa wahitimu wapatao 3,560, wakiwemo wanaume 2,029 na wanawake 1,531. Kati yao, 3,275 walihitimu shahada za kwanza, 127 shahada za umahiri, 18 shahada za uzamivu (PhD), 100 stashahada na 38 astashahada.

Prof. Chibunda alisisitiza kuwa SUA inaendelea kutoa wahitimu wenye ujuzi wa vitendo, wanaoweza kujiajiri, wenye ubunifu na wanaoweza na kuleta tija katika sekta za kilimo, mifugo, maliasili, na maendeleo ya jamii.

Aidha, alieleza kuwa chuo kimeendelea kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia, pamoja na kuimarisha ubora wa mitaala ili iendane na mahitaji ya soko la ajira la sasa na la baadaye.

"Elimu ya SUA inalenga kumwandaa mhitimu anayeweza kufikiri kimkakati, kutumia sayansi na ubunifu wake kuleta mabadiliko kwenye jamii," aliongeza Prof. Chibunda.

Mahafali hayo yalihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali, wanajumuiya wa SUA, na wadau wa elimu, wakiwa na kaulimbiu ya Elimu, Utafiti na Ubunifu kwa Maendeleo Endelevu ya Taifa.










# Elimu ya kilimo ni nguzo kuu kukabiliana na changamoto za chakula na ajira

Serikali imesema kuwa elimu ya kilimo ni nguzo muhimu katika kukabiliana na changamoto za usalama wa chakula, mabadiliko ya tabianchi na suala la ajira kwa vijana.

Akizungumza katika hafla ya ugawaji wa tuzo kwa wanafunzi na watumishi waliofanya vyema kitaaluma, katika utafiti na ubunifu katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Bw. Gerald Mweli, alisema utaratibu huo ni ishara ya safari ndefu ya umahiri, ubunifu na kujituma unaokipambanua chuo cha SUA kama kitovu cha maarifa na mabadiliko.

Alisema kuwa chini ya uongozi wa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, Serikali imeendelea kuwekeza katika programu mbalimbali za kuwawezesha vijana kujijengea uwezo katika kilimo ikiwemo BBT, SUA STEPS na Mpango wa Kukuza na Kuendeleza Kilimo Biashara (AIP). Programu hizi zimekuwa kichocheo muhimu kwa vijana kujiajiri, kuwa wabunifu na kushiriki kikamilifu katika mnyororo wa thamani wa kilimo.

Bw. Mweli aliongeza kuwa SUA ina jukumu kubwa si tu kwa Tanzania bali pia kwa bara zima la Afrika katika kuzalisha wahitimu na watafiti wenye uwezo wa kuchangia katika kuimarisha uzalishaji wa chakula na kuboresha mifumo ya chakula duniani. Vilevile, ameipongeza SUA kwa kupitia upya mitaala yake ili kuendana na mahitaji ya soko la ajira la karne ya 21.

Awali, akimkaribisha mgeni rasmi katika tuzo hizo, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, Prof. Raphael Chibunda, alisema zaidi ya wanafunzi na wanataaluma 180 wamefanya vizuri katika masomo, tafiti na ubunifu mbalimbali, na watatunukiwa zawadi kuanzia shilingi elfu 50 hadi milioni moja.


Prof. Chibunda aliwapongeza wahitimu wote waliopata tuzo hizo na kueleza matumaini yake kwamba wataendelea kufanya vizuri na kuchangia katika kutatua changamoto za jamii wanazotoka.

Kwa upande wake, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo upande wa Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalam, Prof. Maulid Mwatawala, alisema utaratibu huo wa kutoa zawadi ni kichocheo cha kuongeza ari na ufanisi katika masomo, tafiti na ubunifu.

Alisisitiza kuwa kuwatambua na kuwazawadia wanafunzi na wanataaluma wanaofanya vizuri kunasaidia kukuza ushindani chanya na kuleta matokeo bora zaidi chuoni na katika jamii kwa ujumla.








# SUA yaanzisha mageuzi makubwa ya mitaala kuimarisha ujuzi wa vitendo

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kimeanzisha mageuzi makubwa ya mitaala yenye lengo la kuongeza ujuzi wa vitendo kwa wanafunzi na kuandaa wahitimu wenye uwezo wa kutatua changamoto za kijamii kwa kutumia sayansi, teknolojia na ubunifu.

Akizungumza wakati wa mkutano wa SUA CEO Alumni Forum 2025, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo upande wa Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalam, Prof. Maulid Mwatawala, alisema mageuzi hayo ni sehemu ya mkakati wa chuo kuhakikisha elimu inayotolewa inakidhi mahitaji ya soko la ajira na maendeleo ya taifa.

Alisema mafunzo kwa vitendo sasa yamepanuliwa kutoka wiki tano hadi muhula mzima wa masomo, na wataalamu kutoka sekta ya viwanda na biashara wameanza kushirikishwa moja kwa moja katika kufundisha ili kuongeza uzoefu kwa wanafunzi.

Prof. Mwatawala aliongeza kuwa mageuzi hayo yanalenga kuondoa mfumo wa kukariri na mitihani pekee, badala yake kuweka mkazo kwenye tathmini endelevu, kazi za vitendo na tafiti za ubunifu.

Kwa wanafunzi wa shahada za juu, mfumo huo mpya unawahamasisha kujikita katika tafiti na semina zitakazowawezesha kuchambua na kutatua changamoto za kijamii kwa kutumia mbinu za kisayansi na kiteknolojia.

Alisema mageuzi haya ni sehemu ya dira ya SUA ya kuhakikisha wahitimu wake wanakuwa wabunifu, wachambuzi, na wenye uwezo wa kufanya kazi kwa ufanisi katika mazingira yanayobadilika kwa kasi duniani.













# Wananchi wa Mpimbwe waiomba SUA iwashauri namna sahihi ya kilimo bora cha mpunga

Wananchi wa Kata ya Kasansa, Mpimbwe wamewaomba wataalamu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kuwashauri wakazi wa maeneo hayo namna sahihi ya kulima mpunga pamoja na kujua mbegu nzuri na teknolojia za kilimo.

Ombi hilo lilitolewa na Bi. Naomi James kutoka Kikundi cha Upendo Wanawake wa Iziwasungu akizungumza wakati wa utambulisho wa Mradi wa TAGDev 2.0 AGRIFOSE–RIH, unaotekelezwa chini ya RUFORUM kwa ufadhili wa Mastercard Foundation ukishirikiana na SUA pamoja na Vyuo vingine nchini.

Naomi alisema wananchi wanakosa elimu sahihi katika kilimo cha mpunga, uchaguzi wa mbegu na teknolojia nyingine za kilimo, akisema kupitia utambulisho huo anaona mwanga wa kilimo kwa siku za usoni.

Wakati huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe Bi. Shamim Mwariko aliwataka vijana wa Mpimbwe kutumia mradi wa TAGDev 2.0AGRIFOSE-RIH kutoka SUA kuongeza uzalishaji ili kupata fursa ya masoko ya ndani na nje ya Tanzania.

"Mradi huu ni mradi wa kipaumbele kwetu (Mpimbwe), ni nafasi yetu kuhakikisha tunautumia mradi kuendelea kuimarisha uchumi wa wakulima wetu", alisema.

Mradi wa TAGDev 2.0 AGRIFOSE–RIH ni sehemu ya Programu ya RUFORUM inayotekelezwa kwa ushirikiano kati ya SUA, UDSM, Chuo cha Nelson Mandela na Jukwaa la Vyuo Vikuu Afrika (RUFORUM) kwa ufadhili wa Mastercard Foundation ni mradi wa miaka-Mitano na una thamani ya Shilingi Bilioni 1.6.



# Uandishi wa machapisho ya kisayansi upewa kipaumbele SUA

Watafiti, wahadhiri na wanafunzi wa Shahada za Uzamili na Uzamivu wametakiwa kuzingatia uandishi wa machapisho ya kisayansi yenye ubora wa kimataifa ili kuongeza tija ya tafiti na kuimarisha hadhi ya vyuo vikuu vya Afrika katika majukwaa ya kitaaluma.

Wito huo ulitolewa katika mjadala wa kitaaluma ulioandaliwa na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kupitia Mradi wa NANO COM unaolenga kuboresha uelewa na ubora wa uandishi wa kisayansi.

Prof. Gaymary Bakari, Kiongozi wa Mradi wa NANO COM na Naibu Rasi wa Ndaki ya Tiba ya Wanyama na Sayansi za Afya (SUA), alisema uandishi wa kisayansi ni ujuzi muhimu kwa kila mtafiti kwani ndio kipimo cha kazi ya kitaaluma.

Alisema mradi huo unalenga kuwajengea uwezo watafiti ili waandike machapisho yenye viwango vya kimataifa, jambo litakaloongeza ubora wa tafiti kutoka SUA.

Kwa upande wake, Prof. Xin Zhao kutoka Chuo Kikuu cha McGill, Canada, alisisitiza kuwa ubora wa elimu na tafiti za kisayansi ndio msingi wa maendeleo ya taifa, na kwamba nchi zilizoendelea zimepiga hatua kwa kuwekeza katika elimu na utafiti.

"Katika nchi nyingi zilizoendelea, wanafunzi hawawezi kuhitimu bila kuchapisha makala katika majarida yenye viwango vya juu," alisema Prof. Zhao.

Aliongeza kuwa uandishi wa kisayansi unapaswa kuwa wazi, sahihi na wenye ushahidi.

"Uandishi wa kisayansi sio kama riwaya; unahitaji hoja zenye uthibitisho. ChatGPT inaweza kusaidia kuhariri maandiko, lakini haiwezi kufanya majaribio ya kisayansi, hivyo tumieni teknolojia kwa busara," alisema.

Aidha, aliwasihi watafiti wachanga kuepuka kurudia tafiti zilizowahi kufanywa na kujikita katika tafiti zenye ubunifu na mchango halisi kwa jamii.












# SUA yalipa fidia ya Bilioni 1.7 Mpimbwe mkoani Katavi

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kimelipa fidia ya ardhi ya shilingi za kitanzania Bilioni 1.7 kwa wananchi wa maeneo ya Kibaoni katika Halmashauri ya Mpimbwe mkoani Katavi.

Akizungumza katika hafla ya utoaji fidia hiyo Kaimu Mkurugenzi wa Kurugenzi ya Mipango na Maendeleo Chuo Kikuu cha Sokoine Cha Kilimo SUA Dkt. Felix Nandonde alisema jumla ya wafidiwa 197 wamenufaika na malipo hayo.

Alisema SUA iliona kuna umuhimu wa kupanua shughuli zake kwa kuongeza maeneo baada ya kuanzisha Kampasi ya Mizengo Pinda Mkoani Katavi, Kampasi iliyoazishwa mwaka 2019 baada ya kupewa na Halmashauri ya wilaya ya Mpimbwe maeneo yenye ukubwa wa ekari 64 yenye majengo na ekari 200 zilizoko kitongoji cha Vilolo kilomita 8 kutoka chuoni.

Akizungumza katika hafla ya zoezi la kulipa fidia hiyo Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Prof. Raphael Chibunda aliishukuru Serikali kwa kukubali kulipa fidia ili kuongeza eneo la Chuo hicho katika Kampasi ya Mizengo Pinda.

"Mimi nimefanya kazi Serikali Kuu kwa miaka 8 kabla ya kuja SUA, mara nyingi ukiwa kwenye kipindi cha uchaguzi na huu ndiyo mwezi wa uchaguzi, siyo rahisi kwa Serikali kutenga fedha kwa ajili ya kufanya tukio tunaloenda kulifanya leo, kwa hiyo tutambue kuwa huu ni muujiza ambao Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ametutendea" alisema Prof. Chibunda

Naye Mkuu wa Mkoa wa Katavi Mhe. Mwanamvua Mrikondo alisema Serikali inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu ina nia ya dhati ya kuhakikisha inawahudumia wananchi katika nyanja zote ikiwemo elimu na kilimo.

Alisema Serikali imetoa kiasi hicho cha fedha ili kulipa wananchi na kuhakikisha Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kinakuwa na eneo la kutosha ili kuwa na uwezo wa kudahili wanafunzi wengi zaidi.

Katika hatua nyingine Mhe. Mrindoko aliwataka wanufaika kuhakikisha fedha hizo zinawanufaisha wafaidika na hazivurugi amani katika familia zao bali ziwe chachu ya maendeleo huku akiwatahadharisha kuwepo kwa matapeli ambao hujitokeza mara tu mtu anapopata fedha.

Malipo hayo ya fidia ya mali, ardhi na kifuta machozi kwa makaburi 18 kililipwa kwa wananchi 197 kutoka vitongoji vya Ndemanilwa, Kakuni na Lalanayo wanaoishi katika Halmashauri ya Mpimbwe ambao wanapisha upanuzi wa chuo kwenye eneo lenye ukubwa wa jumla ya ekari 690 sawa na hekta 279.

# Wanafunzi watatu SUA wang'ara tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari za Sayansi Tanzania

Wanafunzi watatu wa Shahada ya Uzamili ya Taarifa na Menejimenti ya Maarifa (MIKM) kutoka Idara ya Infomatiki na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (DIIT) ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) wameng'ara kwenye tuzo kubwa zinazotambua mchango wa wanahabari kwenye kuandika taarifa za sayansi na bioteknolojia Afrika kwa upande wa Tanzania (OMAs).

Wanafunzi hao ni Rebecca Kachembeho na Jackline Martine ambao wameibuka kwa pamoja washindi wa jumla wa tuzo hizo (Overall winner) kwa kuandika taarifa nzuri iliyohusu nafasi ya bioteknolojia kwenye kutatua changamoto za ugonjwa mnyauko wa migomba Mkoani Kagera, Changamoto za wadudu wa Pamba wanaokwamisha tija pamoja na makala kuhusu Bungua wa Mahindi na Viwavijeshi vamizi wanavyorudisha maendeleo ya wakulima nchini.

Mwandishi mwingine ambaye pia ni Mwanafunzi aliyeng'ara kwenye tuzo hizo ni Martinius Sospeter ambaye ameshika nafasi ya pili kwa upande wa magazeti kwa kuandika Makala nzuri iliyoonesha mchango wa Sayansi hasa Bioteknolojia katika kutatua changamoto za upungufu wa chakula zinazosababishwa na mabadiliko ya tabia nchi, wadudu na magonjwa na nafasi ya Bioteknolojia katika kuboresha afya nchini Tanzania.

Akizungumza kwa niaba ya washindi na washindi wote kwenye hafla hiyo iliyofanyika jijini Dar es salaam Mshindi wa jumla Bi. Rebecca Kachembeho alikishukuru Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kwa kufundisha kozi ya namna ya kuandika habari za sayansi na kutafsiri matokeo ya kisayansi kwa lugha rahisi kwa jamii ili waweze kuelewa na kutumia matunda ya sayansi.

"Tunakishukuru Chuo Chetu cha Sokoine cha Kilimo kwa kuona umuhimu wa kutufundisha kozi hii na kutupatia mbinu nyingi za namna ya kuwasilisha mada za sayansi kwa jamii, hakika imetupatia mbinu nyingi na maarifa ya kutuwezesha sasa kuitumikia jamii yetu vizuri kwa kuwafikishia matokeo ya tafiti kwa lugha rahisi ili wayatumie kutatua changamoto zinazowakabili na kuongeza ustawi wao katika nyanja mbalimbali." Alisema Bi. Kachembeho.









# Tafiti zichochee kilimo Ikolojia kwa maendeleo endelevu

Wadau wa kilimo ikolojia kutoka taasisi mbalimbali nchini wamekutana katika Warsha ya Kitaalamu iliyoandaliwa na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), kupitia Kitengo cha Kilimo Endelevu (Agroecology Hub in Tanzania – AEHT).

Warsha hiyo ilihusisha miradi miwili ya utafiti ya Regional Multi-actor Research Network on Agroecology in East Africa (RMRN-EA) na Research for Agroecology Network Southern Africa (RAENS), yenye lengo la kujadili uboreshaji wa mitaala ya elimu ya kilimo ikolojia nchini.

Akifungua warsha hiyo kwa niaba ya Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. Raphael Chibunda, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo upande wa Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalam, Prof. Maulid Mwatawala, alisema kuwa upanuzi wa tafiti katika eneo la kilimo ikolojia utachochea maendeleo makubwa ya kitaaluma na kiuchumi.

"Upanuzi wa tafiti katika eneo la kilimo ikolojia utachochea maendeleo makubwa ya kitaaluma," alisema Prof. Mwatawala, akisisitiza umuhimu wa kuelewa ikolojia yenyewe kama njia endelevu ya kuongeza tija katika kilimo.

Aidha, Prof. Mwatawala alibainisha kuwa tafiti nyingi zimeonyesha mapengo katika ulinzi wa mazao, hasa katika udhibiti wa wadudu, hivyo ni muhimu kuanzisha Kituo cha Umahiri (Centre of Excellence) cha kilimo ikolojia SUA ili kukuza utafiti na mafunzo katika eneo hilo.

Kwa upande wake, Prof. Japhet Kashaigili, ambaye ni Mkurugenzi wa Kurugenzi ya Shahada za Uzamili, Utafiti, Uhaulishaji wa Teknolojia na Ushauri wa Kitaalamu na Kiongozi wa Mradi wa RMRN-EA kutoka SUA, alisema kuwa utafiti huo unalenga kuchunguza jinsi masuala ya kilimo ikolojia yanavyowekwa kwenye mitaala kuanzia shule za msingi hadi elimu ya juu.

"Lengo ni kupata taswira kamili ya jinsi elimu ya kilimo ikolojia inavyotekelezwa nchini, ili kubaini mapengo yaliyopo na kuandaa mitaala bora zaidi," alisema Prof. Kashaigili.

Naye Prof. Dismas Mwaseba, Kiongozi wa Mradi wa RAENS na Mtafiti Mwandamizi kutoka SUA, alieleza kuwa warsha hiyo inalenga kufanya tathmini ya utekelezaji wa elimu ya kilimo ikolojia nchini na kwamba matokeo ya utafiti yatachangia katika uboreshaji wa mitaala inayojibu changamoto na fursa zilizopo kwenye sekta ya kilimo.

Kwa upande wake, Bw. Abdallah Ramadhan, Mratibu wa Tanzania Alliance for Biodiversity (TABIO), alisema kuwa mitaala hiyo ikikamilika itawawezesha wanafunzi kutoka taasisi mbalimbali za elimu kupata ujuzi wa kuwaelimisha wakulima na jamii kuhusu mbinu endelevu za kilimo.







# Elimu ni msingi wa kudhibiti mabadiliko ya tabianchi



Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Mhe. Musa Kilakala, amesema mabadiliko ya tabianchi yameendelea kuathiri kwa kiwango kikubwa ustawi wa jamii na mazingira, hivyo kuwataka wananchi kuacha tabia ya uchomaji moto kwenye milima, uharibifu wa vyanzo vya maji na kutofanya shughuli za kibinadamu katika maeneo yasiyostahili ili kulinda mustakabali wa mazingira.

Akizungumza baada ya kufunga Kongamano la Pili la Kisayansi la Muungano wa Vyuo Vikuu Vitano lililofanyika mjini Morogoro, Kilakala pia alikishukuru Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kwa kuwa mwenyeji wa kongamano hilo muhimu na kusema SUA imeonesha uongozi na dhamira kubwa katika kushirikiana na vyuo vikuu vingine na wadau wa kimataifa kujadili masuala ya tabianchi na maendeleo endelevu.

"Msingi wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ni elimu, hivyo jamii nzima inapaswa kushirikiana katika kuelimisha wananchi ili wajue athari za vitendo vyao kwa mazingira kwani jukumu la kulinda mazingira si la Serikali pekee, bali ni la kila mmoja", alisema Kilakala.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Kurugenzi ya Uzamili, Utafiti, Uhaulishaji wa Teknolojia na Ushauri wa Kitaalamu ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya Kongamano hilo, Prof. Japhet Kashaigili kutoka SUA, alisema kongamano hilo limeweka maazimio muhimu yatakayotekelezwa kwa vitendo.

Miongoni mwa maazimio hayo ni kuendeleza programu za ubadilishanaji wa wanafunzi na walimu ili kujenga uwezo wa pamoja, kuanzisha vituo vya teknolojia na ubunifu, pamoja na kuandika maandiko ya pamoja ya utafiti yanayolenga kutoa suluhisho la changamoto



# Wataalam wa lugha kutoka Cuba waanza kufundisha Kihispania SUA, kuongeza nguvu katika ushirikiano wa kimataifa

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kimepokea wataalam wawili wa lugha kutoka nchini Cuba, watakaofundisha lugha ya Kihispania kwa kipindi cha miaka miwili chini ya Idara ya Lugha, katika jitihada za kuendeleza elimu ya kimataifa na kuboresha umahiri wa lugha miongoni mwa wanafunzi.

Akizungumza wakati wa hafla ya kuwapokea, Mratibu wa Kitengo cha Umataifishaji na Majalisi wa SUA, Prof. Jonathan Mbwambo, alisema ujio wa wataalam hao ni sehemu ya muendelezo wa ushirikiano wa muda mrefu kati ya Tanzania na Cuba, unaolenga kuimarisha elimu, utafiti na urafiki wa kimataifa.

Alisema SUA inatambua umuhimu wa lugha ya Kihispania katika mawasiliano ya kimataifa na inahamasisha wanafunzi kutumia fursa hiyo kujifunza lugha hiyo, ambayo ni miongoni mwa lugha zinazozungumzwa zaidi duniani.

Kwa upande wao, wataalam hao, Bi. Yusimí Vigoa Maruri na Bw. Lazaro Nochea Vilella, walieleza kufurahishwa na mapokezi mazuri waliyoyapata SUA pamoja na fursa ya kushirikiana na walimu na wanafunzi katika kukuza elimu ya lugha na tamaduni.

Bi. Maruri alisema wamejipanga kuhakikisha wanafunzi wa SUA wanapata ujuzi wa kina wa lugha ya Kihispania na uelewa wa tamaduni za Cuba na Amerika ya Kusini, wakiamini kuwa ni msingi muhimu katika mawasiliano ya kimataifa na fursa za ajira duniani.



# Ugonjwa wa homa ya kiwele hupunguza mapato ya wafugaji wa ng'ombe wa maziwa

Wafugaji wa ng'ombe wa maziwa barani Afrika, hususan nchini Tanzania, wameendelea kukabiliwa na upungufu wa mapato kutokana na ugonjwa wa homa ya kiwele (mastitis) unaoathiri uzalishaji na ubora wa maziwa.

Ugonjwa huu umekuwa changamoto kubwa kwa wafugaji kutokana na gharama kubwa za matibabu pamoja na kupungua kwa ufanisi wa dawa zinazotumika kukabiliana nao.

Hayo yalibainishwa katika utafiti unaoendelea kufanywa na watafiti kutoka SUA chini ya uongozi wa Prof. Gaymary Bakari, kupitia mradi unaolenga kuchunguza hali ya maambukizi ya homa ya kiwele na usugu wa vimelea vinavyosababisha ugonjwa huo dhidi ya dawa.

Kwa mujibu wa Profesa Bakari, homa ya kiwele ni ugonjwa unaoathiri sehemu ya kiwele cha ng'ombe wa maziwa na husababishwa na vimelea, majeraha, uchafu au lishe duni.

Athari zake ni kubwa, zikiwemo kupungua kwa uzalishaji wa maziwa, kushuka kwa ubora wake, na ongezeko la gharama za matibabu kwa wafugaji.

"Changamoto kubwa tuliyonayo sasa ni ongezeko la vimelea sugu kwa dawa zinazotumika mara kwa mara kama penicillin, oxytetracycline na sulphadimidine. Hali hii inaongeza gharama za matibabu na kupunguza ufanisi wa tiba," alieleza Profesa Bakari.

Mradi huo ujulikanao kama NANO COM unatekelezwa katika mikoa ya Tanga, Iringa, Mbeya, Njombe na Arusha, ambapo tafiti zinafanyika ili kubaini vyanzo vya maambukizi ya homa ya kiwele na kubuni tiba mbadala, salama na nafuu zitakazowanufaisha wafugaji wa ng'ombe wa maziwa nchini Tanzania.







# SUA yajipanga kutoa wahitimu wenye ujuzi na wenye kuendana na mahitaji ya soko

Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, (Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalam), Prof. Maulid Mwatawala, amesema mabadiliko ya mitaala ya SUA yanalenga kuandaa wahitimu watakaokuwa na uwezo wa vitendo na uelewa mpana wa mazingira ya kazi.

Alisema mfumo mpya wa ufundishaji utahusisha zaidi wataalamu kutoka sekta za uzalishaji kama viwandani na mashambani, ambao watashiriki moja kwa moja katika ufundishaji ili kuongeza uhalisia na uzoefu wa kazi kwa wanafunzi.

Prof. Mwatawala aliongeza kuwa kwa sasa wanafunzi wa SUA watafanya mafunzo ya vitendo kwa kipindi cha semista nzima badala ya wiki tano za awali, ili waweze kuzoea mazingira ya kazi na kujifunza stadi muhimu. “Tunataka mwanafunzi atoke chuoni akiwa tayari anajua kufanya kazi,, siyo tu anafahamu kwa nadharia,” alisema.

Kwa upande wake, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo (Mipango, Fedha na Utawala), Prof. Amandus Muhairwa, aliwataka wahadhiri wa SUA kuonesha kwa vitendo wanachofundisha ili kuwasaidia wanafunzi kupata matokeo halisi ya mafunzo.

“Ni wakati wa kutenda, siyo kulalamika. Tuna rasilimali na wataalamu, tukitenda, matokeo yataonekana,” alisisitiza Prof. Muhairwa.

Warsha hiyo imeandaliwa kupitia mradi wa TAGDev 2.0 AGRIFOSE–RIH, unaotekelezwa kwa ushirikiano kati ya SUA, UDSM, Nelson Mandela (NM-AIST), na RUFORUM kwa ufadhili wa Mastercard Foundation.







# Vijana washauriwa kutumia maarifa yanayotolewa SUA kujiinua kimaisha



Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ifakara Mjini Said Majaliwa amewaeleza vijana nchini kutumia uwepo wa SUA kama kitovu cha elimu ya kilimo kwani dunia ya sasa inahitaji maarifa sahihi ili kupata matokeo mazuri katika mavuno.

Alisema hayo wakati wa ufungaji wa mafunzo ya Mradi wa TAGDev 2.0AGRIFOSE-RIH kwa vikundi vinne vya vijana kutoka Ifakara ambapo amewasihi vijana kutumia wingi wa maarifa kutoka Chuo Kikuu Cha Sokoine cha kilimo ili kufanikiwa katika uzalishaji wenye tija.

"Vijana wa Ifakara sasa wakati wenu wa kuinuka Kiuchumi zingatieni elimu iliyotolewa na SUA", alisema Majaliwa.

Naye, Mwenyekiti wa Kikundi cha Umoja wa Mafundi Ujenzi Kiberege Bwawani ambao wanajihusisha na kilimo cha mpunga alisema wamekuwa wakikabiliwa na changamoto ya kupata mavuno hafifu huku wakitumia nguvu nyingi ambapo amewaomba SUA kuwasaidia kutatua changamoto ya mitaji midogo, matumizi ya viwatilifu kutokana na dawa zingine kugoma kutibu ugonjwa unapotokea na kupata soko la uhakika.

Kwa upande wake Kiongozi Mshiriki wa Mradi huo, Dkt. Nyambilila Amuri, alisema mradi upo kwa miaka mitano vijana watashiriki kikamilifu katika kupanua mnyororo wa thamani katika sekta ya kilimo katika kulenga kuwashawishi na kuwahamasisha kujiunga na kuwekeza katika kilimo kwa kuwapatia mazingira rafiki na teknolojia.



# Warsha ya uzinduzi wa Mradi wa Mtandao wa Wadau wa Utafiti wa Kilimo Ikolojia kwa Afrika Mashariki (RMRN-EA) inalenga Kuimarisha kilimo ikolojia Afrika Mashariki.

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kimezindua mradi wa Mtandao wa Wadau wa Utafiti wa Kilimo Ikolojia kwa Afrika Mashariki kupitia warsha ya siku moja iliyofanyika chuoni hapo, ikihusisha watafiti, watunga sera, wakulima na wadau mbalimbali. Warsha hiyo imejikita katika kuimarisha utafiti wa kilimo ikolojia (agroecology) na kuongeza ushirikiano kati ya taasisi za elimu, utafiti, wakulima na jamii.

Akizungumza wakati wa uzinduzi, Prof. Japhet Kashaigili, Kiongozi wa Mradi wa RMRN-EA, alisema mradi huo umelenga kuendeleza mitaala ya agroecology, kujenga mtandao wa utafiti na kubadilishana taarifa kati ya nchi washiriki.

Amesema mradi utasaidia kukuza ushiriki wa wanawake zaidi ya asilimia 30 katika shughuli zote za mradi.

Kwa upande wake, Prof. Maulid Mwatawala, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalam, alipongeza mradi kwa kuzingatia vipengele vinavyohakikisha ufanisi wake.

Alieleza kuwa mradi unajumuisha usawa wa kijinsia na ushirikishwaji wa wadau, unaweka mkazo katika uendelevu hata baada ya muda wa ufadhili kuisha, unajikita katika muktadha wa kikanda na kitaifa kupitia ushirikiano wa nchi washiriki, na unaendana na sera na ajenda kubwa za kimataifa ikiwemo SDGs, AU Agenda 2063 na CAADP.

Mradi wa RMRN-EA unatekelezwa kwa ushirikiano wa vyuo vikuu vya Afrika Mashariki, ikiwemo Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kwa upande wa Tanzania, Chuo Kikuu cha Makerere, Uganda, na Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya.

# Ubunifu na Utafiti nguzo za maendeleo ya jamii

Mshikamano wa kitaaluma, ubunifu na utafiti kati ya vyuo vikuu nchini umetajwa kuwa ni nguzo muhimu katika kuzalisha matokeo chanya kwenye sekta ya elimu na kuimarisha maisha ya jamii kwa kushughulikia changamoto mbalimbali.

Hayo yalisemwa na Prof. Japhet Kashaigili, Mkurugenzi wa Kurugenzi ya Uzamili, Utafiti, Uhaulishaji wa Teknolojia na Ushauri wa Kitaalamu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya Kongamano la Pili la Kisayansi la Muungano wa Vyuo Vikuu Vitano, linaloendelea mjini Morogoro.

Prof. Kashaigili alisema kongamano hilo limekusanya takribani washiriki 200 kutoka vyuo vikuu vitano vya ndani na nje ya nchi, vikiwemo SUA, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Aga Khan, Chuo Kikuu cha Nelson Mandela na Chuo Kikuu cha Simon Fraser cha Canada. Ushirikiano huo unatokana na makubaliano ya kitaaluma na utafiti yaliyowekwa na taasisi hizo.

"Lengo la kongamano hili ni kubadilishana uzoefu wa kitaalamu, kuimarisha uwezo wa walimu na wanafunzi, pamoja na kuandaa machapisho ya pamoja ya tafiti yatakayosaidia kutafuta suluhisho la changamoto za kijamii," alisema Prof. Kashaigili.

Aliongeza kuwa ubunifu unaotokana na tafiti hizo una mchango mkubwa katika kuongeza tija ya kilimo, kuboresha huduma za afya na upatikanaji wa maji safi, pamoja na kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi kupitia suluhisho za kitaaluma na kiteknolojia.

Kongamano hilo pia lilitoa nafasi kwa watafiti chipukizi kuwasilisha tafiti zao na kujenga mitandao ya kitaaluma, hatua ambayo itachochea ushirikiano endelevu na kuhakikisha matokeo ya tafiti yanakuwa na manufaa kwa taifa na dunia kwa ujumla.

Kongamano la mwaka huu limebeba kaulimbiu inayosema: "Zaidi ya Kuishi: Kujenga Jamii Shirikishi na Zinazostahimili Mabadiliko ya Tabianchi."










# SUA yawapa elimu na pongezi wanafunzi wa mwaka kwanza 2025/2026

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali ikiwemo Ofisi ya Uhamiaji mkoani Morogoro, kimetoa elimu na kuwapongeza wanafunzi wa mwaka wa kwanza waliojiunga na chuo hicho kwa mwaka wa masomo 2025/2026.

Akizungumza katika mkutano uliofanyika katika Kampasi ya Edward Moringe Sokoine, November 17 2025 Kaimu Mkuu wa Kitengo Cha Mawasiliano na Masoko wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha kilimo Bi. Suzana Magobeko, aliwapongeza wanafunzi hao na kuwataka kuwa mabalozi wazuri wa chuo, hususan kupitia mitandao ya kijamii.

Aidha, Kaimu Mkuu Mlezi wa Idara ya Ushauri kwa Wanafunzi SUA, Bi. Hilda Gamuya, alisema kuwa mwitikio wa wanafunzi wa mwaka huu ni mzuri tofauti na mwaka wa masomo 2024/2025, kwani wana imani kuwa elimu wanayoitoa inaweza kuleta hamasa na mtazamo chanya ili kuendana na utaratibu wa chuo.

Bi. Hilda aliongeza kuwa matarajio yao makubwa ni kuona wanafunzi wanabadilika na kuendana na utaratibu, sheria na kanuni za chuo, lengo likiwa ni kuwajengea misingi bora ya maisha wawapo katika kampasi chuoni hapo.

Kwa upande wake, Afisa Usajili wa Mkoa wa Morogoro, Bw. James Malimo, alieleza umuhimu wa wanafunzi kuwa na namba ya NIDA, akisema kuwa namba hiyo itawasaidia kupata huduma mbalimbali ikiwemo huduma za afya, mikopo, pamoja na kuepusha usumbufu wa kukosa huduma muhimu kwa wakati.pia itawasaidia kutambulika

Aidha, Bw. James alitoa wito Kwa wanafunzi hao kutoa taarifa sahihi wakati wa mchakato wa usajili, kwani taarifa hizo zitawasaidia katika masuala ya elimu na maisha yao kwa ujumla. na kuwataka wajitokeze kwa wingi kujisajili.

Nao wanafunzi wa mwaka wa kwanza, Bi. Laisa Bakari na Robert Laurent, walieleza namna walivyopokelewa chuoni hapo, wakisema mapokezi yao yamekuwa mazuri na kwamba elimu waliyopewa itawasaidia kufuata sheria, kanuni na utaratibu wa chuo. Aidha, walisema matarajio yao ni kuanza masomo yao rasmi kwa mafanikio.











# TRA yaitembelea SUA kujifunza kuhusu uwekezaji katika kilimo

Watumishi kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ambao wanakaribia kustaafu wamekitembelea Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kwa lengo la kujifunza na kupata elimu ya uwekezaji katika sekta ya kilimo ikiwa ni maandalizi ya maisha baada ya kustaafu.

Akizungumza na wafanyakazi hao baada ya kufika chuoni, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalam Prof. Maulid Mwatawala alisema kuwa SUA imekuwa na ushirikiano wa taasisi mbalimbali nchini ikiwemo TRA mkoa wa Morogoro kwa kutoa mafunzo kuhusu sekta ya kilimo ili kuleta faida kwa taifa.

Aidha, aliwakaribisha SUA na kutoa shukrani zake kwa Mamlaka hiyo kwa kuamua kuitembelea na kujifunza kupitia wataalamu wa SUA ambapo amesema Chuo kitaendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi na marefu katika Nyanja ya kilimo, ufugaji na uvuvi.

Kwa upande wao, wastaafu hao watarajiwa kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania Mkoa wa kodi Temeke Bw. Tilson Kabuje na Bi. Frida Ndyetabula waliipongeza SUA kwa kutoa elimu bora ya kilimo na wamebainisha wazi matarajio yao makubwa baada ya kupokea elimu kuhusu namna ya kuwekeza katika kilimo ili kujikwamua kiuchumi baada ya kustaafu.

“Tumeichagua SUA kwa sababu ni sehemu pekee ambayo tuliona tutapata maarifa na ujuzi ambao utatusaidia kwenye maisha yetu hasa kipindi hiki tunachoelekea kuhitimisha safari ya utumishi wetu”, alisema Bi. Frida.

Watumishi hao kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania walitembelea Shamba la Mafunzo katika Kitengo cha Samaki, Kitengo cha Mifugo na Nyanda za Malisho, Kitengo cha Mimea Vipando kinachojihusisha na uzalishaji wa miche ya matunda mbalimbali.





# SUA imeenda na kasi ya mabadiliko ya sera ya elimu - TCU

Mkurugenzi wa Ithibati kutoka Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) Dkt. Telemu Kassile amekipongeza Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kwa kuendana na kasi ya mabadiliko ya Sera mpya ya Elimu ya 2023 inayosisitiza mitaala ya sasa ambayo itawapa wahitimu ujuzi wa kuweza kuajiriwa au kujiari popote watakapokuwa mara baada ya kuhitimu masomo yao.

Akifungua warsha Mkoani Morogoro Dkt. Kassile alisema SUA wameandaa mafunzo ya siku 5 ya kuwajengea uwezo wanataaluma na viongozi mbalimbali katika ngazi tofauti tofauti SUA mara baada ya kuhuisha mitaala yake, na kutengeneza mitaala mipya iliyozingatia hali halisi.

"Pongezi SUA, wanaenda na kasi ya mabadiliko Mafunzo haya yanalenga zaidi katika kuwapa mbinu washiriki ya namna ya kufundisha mitaala iliyofanyiwa marejeo baada ya sera ya elimu na mafunzo ya mwaka 2014 kufanyiwa mapitio na kutolewa toleo la mwaka 2023 kwa kuwa sera hiyo imesisitiza zaidi wahitimu kuweza kuwa na na ujuzi na sisi TCU kama wasimamizi tulitoa maelekezo kwa vyuo vikuu vyote nchini kuhuisha mitaala yao na wanaoandaa mitaala mipya waweze kuandaa mitaala ambayo itawapa wahitimu ujuzi wa kuweza kuajiriwa au kujiari" alisema Kassile.

Kwa upande wake, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Cha Sokoine cha Kilimo upande wa Taaluma ,Utafiti na Ushauri wa Kitaalam Prof. Maulid Mwatawala alisema, wanafunzi wa SUA watanufaika na utekelezaji wa mabadiliko ya sera kwa kuboresha kuanzia utoaji wa mafunzo ambao kwa sasa utabadilika kwa kuongeza watu wanaotoka kwenye viwanda na sehemu zingine za kazi ambao wanauzoefu na siyo waalimu wa SUA pekee ambao watakuja na stadi walizonazo na ufundishaji sambamba na ufundishaji wa kidigijiti.

Aliongeza kuwa Sehemu kubwa ya mafunzo kwa sasa mwanafunzi ataweza kujifunza wenyewe na kushirikiana na wenzake tofauti na mfumo wa zamani ambao mwalimu alisimama mbele na kufundisha kile anachojua sanjari na mabadiliko katika mfumo wa mafunzo kwa vitendo ambapo kwa sasa mwanafunzi mwaka wa mwisho atakaa sehemu ya mafunzo ya vitendo kwa semista nzima ili ajifunze stadi za kazi na mazingira ya kazi ili akimaliza anakuwa tayari kuanza kazi tofauti na mfumo wa zamani mwanafunzi alikuwa anaenda mafunzo kwa vitendo kwa wiki 5.

Nae Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Mipango, fedha na Utawala, Prof. Amandus Muhairwa alisema katika mafunzo haya wanawataka wataalamu wote wa SUA wafanye wanachoongea kwa vitendo ili mwanafunzi aone uhalisia wake akijua hiyo ndio ajira yake na vile vile wataalamu hao kuwasukuma wanafunzi katika kutenda zaidi uhalisia wa kupata matokeo.

"Muda wa kulalamika umekwisha hatuna sababu tena kwa sasa tuna rasilimali zote, mali na watu wamesoma wana ujuzi mkubwa ni wakati wa kutenda siyo kulalamika wala kutafuta ubaya uko wapi na wapi ,ni wakati wetu kutenda na inawezekana kila mtu akitimiza wajibu wake" alisema Prof. Muhairwa.



# Mchango wa ufugaji wa kuku kuondoa umaskini

Mafunzo ya ufugaji bora wa kuku kwa wafugaji 23 ku toka mikoa mbalimbali nchini, yamemalizika Novemba 20 katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA, yakilenga kuongeza uzalishaji wa mayai na nyama pamoja na kuboresha lishe ya jamii.

Akifunga mafunzo hayo kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Hilary Sagala ambaye ni Afisa Tawala alisema ufugaji bora wa kuku una mchango mkubwa katika kupunguza umasikini

Alisema watumishi wengi na wafanyakazi wa sekta binafsi wanapaswa kupata nafasi ya kujifunza ili hata wanapostaafu waweze kuwa na shughuli za kukuza uchumi wao na kupunguza umaskini katika Kaya.

Kwa upande wake, mwakilishi wa Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo ambaye ni Rasi wa Ndaki ya Misitu, Wanyamapori na Utalii Prof. Agnes Sirima alisema SUA itaendelea kushirikiana na taasisi mbalimbali ili kuhakikisha elimu ya kitaalamu inawafikia wafugaji zaidi nchini.

Naye mwakilishi wa Mkurugenzi wa Taasisi ya Elimu ya Kujiendeleza ICE Dkt. Emmanuel
Malisa alisema mafunzo hayo yaliyodumu kwa siku nne yamehusisha nadharia na vitendo, ikiwemo ulishaji wa vifaranga, ujenzi wa mabanda, chanjo na mbinu za biashara.

Kwa upande wake Prof. Tiisekwa Bendantungukwa kutoka AICAD alisema ufugaji wa kuku ni eneo linaloweza kuleta matokeo ya haraka, hivyo elimu hiyo inawajengea uwezo washiriki kuongeza kipato na usalama wa chakula majumbani.

Baadhi ya washiriki walisema mafunzo hayo yamewasaidia kuelewa namna ya kupunguza vifo vya kuku na kupata tija zaidi katika uzalishaji.



# SUA yashirikiana na Ashish Life Science kuwatambua wanafunzi bora wa tiba ya wanyama

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), kupitia Ndaki ya Tiba ya Mifugo na Sayansi za Afya, kimewatambua na kuwatunuku zawadi wanafunzi waliopata ufaulu wa juu katika masomo yao ya tiba ya wanyama, tukio ambalo limefanyika Oktoba 15, 2025, kwa ushirikiano na kampuni ya kimataifa ya dawa za mifugo, Ashish Life Science (ALS), ambayo imekuwa mshirika mkubwa wa SUA kwa miaka mitano mfululizo katika kuinua ubora wa elimu ya tiba ya mifugo nchini.

Akizungumza katika hafla hiyo, Prof. Ezron Karimuribo, Rasi wa Ndaki ya Tiba ya Mifugo na Sayansi za Afya, alisema ushirikiano huo kati ya SUA na ALS umekuwa na manufaa makubwa kwa wanafunzi,

"Kampuni hii imekuwa ikiwatia moyo vijana wetu kwa kuwapatia elimu kuhusu dawa mpya sokoni, kutoa ajira kwa wahitimu wetu, na kuanzisha programu za mafunzo kwa vitendo (internship) zinazowaandaa wanafunzi kwa maisha ya kitaaluma," alisema Prof. Karimuribo.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa ALS Tanzania, Dkt. Sanjeev Sarkar, alisema kampuni hiyo yenye makao makuu nchini India imejikita katika kuhakikisha afya, ustawi, na uzalishaji bora wa wanyama duniani huku akisisitiza kwamba ushirikiano wake na SUA umeendelea kuwa chachu ya kukuza wataalamu wabunifu na wenye ujuzi katika sekta ya mifugo, hivyo kuchangia moja kwa moja katika maendeleo ya uchumi wa Tanzania kupitia afya bora na uzalishaji wa mifugo.

Wakizungumza katika hafla hiyo, baadhi ya wahitimu waliotunukiwa zawadi, akiwemo Martina Charles Mgeni, walieleza kwamba tuzo hiyo ni heshima kubwa na motisha ya kuendelea kufanya vizuri zaidi,

"Ni furaha kwangu kuona chuo kimetambua juhudi zangu kwani hii inanipa hamasa zaidi kuendelea kufanya vizuri katika taaluma ya tiba ya wanyama," alisema Martina kwa furaha.

Katika hafla hiyo, kampuni ya ALS ilitoa zawadi kwa wanafunzi watano bora zaidi katika nyanja mbalimbali, huku pia wanafunzi wa ngazi ya diploma waliosaidia madaktari wa wanyama wakitambuliwa kwa mchango wao mkubwa katika kuboresha huduma za tiba ya mifugo nchini.










# SUA na Mzuri Afrika washirikiana kukuza ujuzi wa vitendo kwa wanafunzi

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kimechukua hatua muhimu katika kuimarisha mafunzo ya vitendo kwa wanafunzi wake wa Uhandisi Kilimo, Uzalishaji Mazao na Kilimo cha Umwagiliaji kupitia utiwaji saini wa hati ya makubaliano na Kampuni ya Mzuri Afrika.

Dkt. Nelson Makange, Mhadhiri wa Uhandisi wa Kilimo SUA, alisema kuwa makubaliano hayo ni sehemu ya mpango wa maboresho ya mafunzo unaolenga kuunganisha nadharia na vitendo ili kuwaandaa wanafunzi kuwa washindani katika soko la ajira.

"Makubaliano haya yanawawezesha wanafunzi wetu kufanya mazoezi ya vitendo kwa kutumia mashine za Mzuri Pro Tiller, jambo linalowaongezea ujuzi wa kiutendaji na kuwafanya wawe tayari kushindana katika soko la ajira," alisema Dkt. Makange.

Wanafunzi Annarose Show (Uhandisi wa Kilimo) na Abdullah Omary Juma (Shahada ya Uzalishaji Mazao) walisema mafunzo ya vitendo yamewasaidia kufahamu tofauti kati ya nadharia na vitendo.


"Kabla ya mafunzo haya tulikuwa tukijifunza zaidi kwa vitabu na darasani. Sasa tunaona jinsi mashine kama hii inavyofanya kazi shambani, jambo linalotupa uelewa mpana wa kilimo cha kisasa," alisema Annarose.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Mzuri Afrika Bw. Shabani Mgonja, alieleza kuwa ushirikiano huo unalenga kuhamasisha matumizi ya teknolojia ya kisasa kwa wanafunzi na wakulima wadogo na kuhakikisha mashine za Mzuri Pro Tiller zinatumika kwa ufanisi nchini.

Makubaliano hayo ni mfano wa ushirikiano wenye tija kati ya vyuo vikuu na sekta binafsi katika kutoa mafunzo ya vitendo, kuongeza ujuzi wa kiufundi na kuchochea maendeleo ya kilimo cha kisasa nchini Tanzania.

Kupitia ushirikiano huo, wanafunzi wa SUA sasa wanapata fursa ya kujifunza kuendesha na kuelewa kwa undani mashine za kisasa za kilimo ujuzi muhimu unaowaandaa kuingia kwa ujasiri katika soko la ajira.








# Ubunifu na uthubutu msingi katika maendeleo

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kimefanya kilele cha maadhimisho ya Siku ya Makamu Mkuu wa Chuo, ikiwa ni sehemu ya kuhitimisha ukaribisho kwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza waliojiunga na SUA kwa mwaka wa masomo 2025/2026.

Tukio hilo lilifanyika katika Ukumbi wa Freedom Squre, Kampasi ya Solomon Mahlangu na kuhudhuriwa na viongozi wa Chuo, wanafunzi na wadau wa elimu.

Akizungumza na wanafunzi hao kwa niaba ya Makamu Mkuu wa Chuo, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo – Taaluma Prof. Maulid Mwatawala alisema Chuo kinaendelea kuboresha mitaala na mifumo ya kujifunzia ili kuendana na sayansi, teknolojia na mahitaji ya soko la ajira ndani na nje ya nchi.

"Tunawataka wanafunzi kujikita katika maarifa, utafiti na ubunifu. fursa za kujipatia uzoefu zipo wazi kwa atakayekuwa makini na uthubutu," alisisitiza.

Katika kulinda ustawi na huduma muhimu kwa wanafunzi, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo (Mipango, Fedha na Utawala) Prof. Amandus Muhairwa alisema Chuo kinaendelea kuongeza uwekezaji katika miundombinu na huduma rafiki kwa wanafunzi, ikiwemo malazi, usalama na TEHAMA.

Kwa upande wake, Mshauri wa Wanafunzi SUA Bi. Hilda Gamuya alibainisha kuwa ofisi yake imejipanga kuimarisha huduma za ushauri nasaha, usalama, pamoja na malezi ya kijamii kwa wanafunzi, hasa wale wa mwaka wa kwanza.

"Tunataka wanafunzi wapya wakaribishwe kwenye chuo chenye kujali ustawi wao kimwili, kiakili na kijamii. Mlangoni kwetu tuko tayari kuwasikiliza na kuwasaidia," alisema.

Alisema uwepo wa programu za mwongozo na klabu mbalimbali utawasaidia wanafunzi kuzoea mazingira ya Chuo kwa haraka na kuongeza ufanisi wa kitaaluma.






# HABARI PICHA:

*Naibu Makamu Mkuu wa Chuo upande wa Mipango, Fedha na Utawala, Prof. Amandus Muhairwa, akifungua mafunzo ya siku tano kwa Watumishi wa Kitengo cha Mawasiliano na Masoko (CMU) yaliyohusu namna bora ya utumiaji na uendeshaji wa runinga. SUA inafungua runinga ili iweze kutangaza shughuli za Chuo pamoja na kuwapatia elimu na taarifa mbalimbali za kilimo wakulima nchini.*















# Nishati jadidifu kuboresha shughuli za kilimo nchini

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, kupitia Mradi wa Nishati, kinaendelea kuwajengea uwezo wataalamu wake pamoja na watalaamu kutoka Manispaa ya Morogoro katika matumizi ya nishati jadidifu kuweka ujumuishi wa mifumo ili kuongeza matumizi haba ya nishati kwa matumizi mbalimbali.

Hayo yalijadiliwa na watalaam kwenye mafunzo yaliyofanyika Kampasi ya Edward Moringe, Novemba 25, 2025 ambapo imeoneshwa kuwa nishati mbadala ya jua (sola) ina nafasi kubwa ya kuunganisha mifumo ya matumizi zaidi ya kuzalisha nishati kama kutumika kwenye kilimo na kutengeneza kivuli kama sehemu ya kuishi mifugo na pia mazao.

Prof. Esron Karimuribo, Mtafiti Kiongozi wa Mradi wa Nishati SUA alisema wanategemea mafunzo hayo yatawapa ujuzi wahadhiri katika kuona umuhimu wa kuboresha mitaala ya kufundishia ili wanafunzi wajue mifumo hii ya nishati mbadala na namna ambavyo inaweza kuwa jumuishi na endelevu kwa muda mrefu huku watalaamu wa Manispaa ya Morogoro kwenda kuwaelimisha wananchi juu ya fursa hiyo.

"Tunajifunza zaidi namna ya kuunganisha mifumo ya nishati `integrated system` ambayo itaongeza ufanisi kwa watumiaji ambapo kwa wananchi inaweza kuwapunguzia gharama tofauti na nishati nyingine ambazo zimezoeleka", alisema Prof. Karimuribo ambaye pia ni Rasi wa Ndaki ya Tiba ya Wanyama na Sayansi za Afya.

Alisema tofauti na mafunzo yaliyofanyika kwa siku zilizopita, mafunzo ya awamu ya hii yamejikita kwenye nishati ya jua ambayo Kampuni ya Studio Santi wamekuwa wakiitumia na wamefika kutoa uzoefu wao kulinganisha na namna ambavyo wamekuwa wakifanya barani Afrika na barani Ulaya kutokea chini ya ufadhili wa Umoja wa Ulaya.

Wakati mwezeshaji wa mafunzo hayo Mhandisi Pauline Tumaini kutokea Kampuni ya Studio Santi alisema nishati ya sola inayo mawanda tofauti tofauti yanayomuwezesha mtumiaji kuingia kuwekeza, akisema kuna eneo la kuwekeza katika mitambo yenyewe, kuwekeza katika kilimo ambapo umeme unaozalishwa kupitia jua unatumika kusukuma maji katika hicho kilimo pamoja na njia nyingine.

Aidha, alisema Tanzania ina mazingira mazuri yanayoruhusu uwekezaji wa nishati jadidifu tofauti na mataifa aliyotembelea akisema endapo kutakuwa na mwitikio chanya unaoweza kuboresha uchumi wa wananchi kutokana na urahisi wa matumizi.

Mradi wa Nishati unatekelezwa nchini Tanzania na vyuo vikuu viwili vya SUA na Mzumbe pamoja vyuo vikuu vingine vya Afrika Mashariki nchini Uganda na Rwanda na vingine barani Ulaya kwenye nchi za Italia na Uhispania.

## HABARI PICHA:

***Timu ya mpira wa miguu pamoja na timu ya mpira wa pete za watumishi wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo zikiwa katika mashindano yaliyoandaliwa na Shirikisho la Michezo la Mashirika ya Umma, Taasisi na Makampuni Binafsi Tanzania (SHIMMUTA) yaliyofanyika katika viwanja mbalimbali mkoani Morogoro kuanzia Novemba 25, 2025 hadi Desemba 06, 2025.***













# MATANGAZO

## KARIBU UTANGAZE NA SUA FM, 101.1

*Kwa Gharama Nafuu*




@sokoineuniversityofagriculture

@SokoineU

*Kwa Mawasiliano piga simu*

**0655424251**
**0655370047**

# UTALII

## KARIBU UTEMBELEE KAMPASI ZA SUA KWA UTALII NA KUJIFUNZA










SOKOINE UNIVERSITY OF AGRICULTURE
1984
ARDHI NI HAZINA

**Jarida limeandaliwa na:**
**Kitengo cha Mawasiliano na Masoko**
**S.L.P 3000, Chuo Kikuu, Morogoro, Tanzania**
**Simu: 255-023-2640006/7/8/9,**
**Baruapepe: communicationandmarketing@sua.ac.tz**